**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS –TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA MTAMA**

**MUHTASARI WA KIKAO CHA KAMATI YA FEDHA, UTAWALA NA MIPANGO KILICHOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA HALMASHAURI TAREHE 25/11/2021**

**KUMB. NA. 53/2021/2022 – WAJUMBE WALIOHUDHURIA**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 01. Diwani Yusufu Abdallah Tipu | - | Kata ya Nyengedi | -Mwenyekiti |
| 02. Diwani Ally Nampanda | - | Kata ya Nyangamara | -Mjumbe |
| 03. Diwani Omari Mohamedi Liveta | - | Kata ya Mnolela | -Mjumbe |
| 04. Diwani Babu M. Omari | - | Kata ya Nyangao | -Mjumbe |
| 05. Diwani Maria Petro Chonde | - | Kata ya Mtama | -Mjumbe |
| 06. Diwani Saidi Mohamedi Kawanga | - | Kata ya Longa | -Mjumbe |

**KUMB. NA. 53.1/2021/2022 – WAJUMBE WASIOHUDHURIA KWA TAARIFA**

01. Mhe. Nape M. Nnauye (MB) - Jimbo la Mtama

**KUMB. NA. 53.1.2/2021/2022 – WATAALAM WALIOHUDHURIA;**

1. Nd. Mahmoud Kimbokota -Kaimu Mkurugenzi Mtendaji (W) -Katibu
2. Nd. Mbaraka Liengite -Kaimu Afisa Ugavi Wilaya
3. CPA Asha Msangi -Kaimu Mweka Hazina Wilaya
4. Nd. Wenceslaus Mbilango -Afisa Maendeleo ya Jamii Wilaya
5. Nd. Msafiri Wanje -Mwanasheria
6. Nd. Simona Charle -Kaimu Afisa Mifugo na Uvuvi Wilaya
7. Nd. Yusufu Chilumba -Kaimu Afisa Elimu Msingi Wilaya
8. Nd. Mustapha Malibiche -Kaimu Afisa Elimu Sekondari Wilaya
9. Nd. Ahmadi Likuku -Kaimu Afisa Mipango Wilaya
10. Nd. Victor A. Shau -Afisa Maliasili na Ardhi Wilaya
11. Nd. Fadhili Livigha -Mwandishi Mkuu
12. Nd. Salma Mbwago -Mwandishi Msaidizi

**KUMB. NA. 54/2021/2022 – KUFUNGUA KIKAO**

Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa mahudhurio mazuri aliwaomba wawe watulivu kujadili dondoo za agenda zilizowasilishwa. Alifungua kikao saa 4.00 asubuhi.

**KUMB. NA. 55/2021/2022 – KUTHIBITISHA AGENDA**

Dondoo za agenda za kikao zilizowasilishwa na kuthibitishwa ni zifuatazo:-

01. Kufungua kikao
02. Kuthibitisha agenda
03. Kusoma na kuthibitisha muhtasari wa kikao cha tarehe 28/09/2021
04. Yatokanayo na muhtasari wa kikao cha tarehe 28/09/2021
05. Taarifa ya Fedha, Mapato na Matumizi mwezi Septemba, 2021
06. Taarifa ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo robo ya kwanza mwaka 2021/2022
07. Taarifa ya manunuzi robo ya kwanza mwaka 2021/2022



Scanned with CamScanner

08. Taarifa ya ukaguzi ndani robo ya kwanza mwaka 2021/2022
09. Taarifa ya shughuli za Utumishi na Utawala robo ya kwanza 2021/2022
10. Taarifa ya Kitengo cha Sheria
11. Kufunga kikao

**KUMB. NA. 56/2021/2022 – KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA TAREHE 2.10.2021**

Muhtasari tajwa hapo juu ulisomwa na kuthibitishwa hatimaye ulisainiwa na Katibu pamoja na Mwenyekiti na kuwa kumbukumbu sahihi ya kikao.

**KUMB. NA. 57/2021/2022 – YATOKANAYO NA KIKAO CHA KAMATI YA FEDHA, UTAWALA NA MIPANGO CHA TAREHE 22.10.2021**

Yatokanayo na kikao cha tarehe 22.10.2021 yaliwasilishwa kama ifuatavyo:-

***Kumb. Na. 45/2021/2022/1*** - Iliagizwa kuwa, Mkurugenzi Mtendaji Wilaya afuatilie ili madeni yote yaliyokusanywa kupitia POS yalipwe na wahusika wanaodaiwa wabainishwe.

***Utekelezaji*** – Agizo limezingatiwa kwa utekelezaji. Orodha ya wahusika iliwasilishwa kwenye kikao. Baada ya kupitia orodha hiyo wajumbe walitaka wahusika wachukuliwe hatua za kisheria ili madeni walipe.

***Kumb. Na. 45/2021/2022/2*** - Iliagizwa kuwa, Mkurugenzi Mtendaji Wilaya atekeleze suala la kununua dawa za chanjo ya kuku na wakabidhiwe Maafisa kilimo ambapo kila akichanjwa kuku mfugaji alipe ushuru wa chanjo.

***Utekelezaji*** - Agizo limezingatiwa. Kwa kipindi cha mwezi Septemba – Desemba huwa ni kipindi cha kuku kuumwa kitoga, hivyo chanjo tutaanza Januari, 2022, kwani hairuhusiwi kuchanja kitoga kwa kuku anayeumwa kitoga

***Kumb. Na. 49/2021/2022/3*** - Iliagizwa kuwa, Mkurugenzi Mtendaji Wilaya aende Kijiji cha Zingatia akafanye kikao na Serikali ya Kijiji kuhusu Nd. Frank Lukanga (VEO) kutokabidhi Ofisi.

***Utekelezaji*** – Agizo limezingatiwa. Mhusika alikuwa mgonjwa hivyo utekelezaji sahihi utatolewa kwenye kikao cha mwezi Desemba, 2021

***Kumb. Na. 51/2021/2022/4*** - Iliazimiwa kuwa, Mkurugenzi Mtendaji Wilaya akutane na afanye kikao na wafanyabiashara wanaochukua mawe katika Kijiji cha Simana.

***Utekelezaji*** – Agizo limezingatiwa. Kikao kilifanyika lakini waliohudhuria walikuwa wawili tu. Ndg. Jenipha hakuhudhuria na deni la nyuma hajalipa. Wajumbe walieleza kuwa, mfanyabiashara huyo (Jenipha) ni msumbufu. Mkurugenzi Mtendaji Wilaya aendelee kufuatilia madeni ya nyuma.

***Kumb. Na. 51/2021/2022/5*** - Iliazimiwa kuwa, Mkurugenzi Mtendaji Wilaya awasiliane na Mkuu wa Wilaya kuhusu mapato ya mawe yaliyochukuliwa na Kampuni ya DANGOTE eneo la Chimbelenje (Mbuta). Pia afuatilie TARURA miundombinu ya Barabara ya Mnolela – Mbuta.

***Utekelezaji*** – Agizo limezingatiwa. Utekelezaji sahihi utatolewa kwenye kikao cha mwezi Desemba, 2021



Scanned with CamScanner

**KUMB. NA. 57/2021/2021 – TAARIFA YA FEDHA, MAPATO NA MATUMIZI MWEZI OKTOBA, 2021**
Taarifa ya fedha, mapato na matumizi mwezi Oktoba, 2021 iliwasilishwa. wajumbe walipewa kabrasha lililoonyesha hali halisi ya mapato na matumizi.

Taarifa ilipokelewa na Mwenyekiti alikaribisha majadiliano. Taarifa hiyo kwa upande wa mapato wajumbe walitaka jitihada na bidii za kufuatilia mapato ya ushuru wa mkaa ziongezwe katika maeneo yote yanayovunwa mazao ya misitu (mkaa). Aidha, wajumbe walipongeza jitihada zinazofanywa katika kufuatilia ushuru wa huduma ya choo Kituo cha Mabasi Mtama ambapo kwa mwezi Oktoba, 2021 kiasi kilichokusanywa kilikuwa ni Tshs 711,500/=.

Baada ya majadiliano ya kutosha,

**ILIAZIMIWA** kuwa, taarifa ya fedha, mapato na matumizi mwezi Oktoba, 2021 ilikubaliwa na kupitishwa.

**KUMB. NA. 59/2021/2022 – TAARIFA YA UTUMISHI NA UTAWALA**
Taarifa ya shughuli za Idara ya Utawala na Utumishi zilizofanyika kipindi cha mwezi Oktoba, 2021 ziliwasilishwa. Shughuli zilizofanyika ni pamoja na Uimarishaji wa Utawala Bora, Uboreshaji wa Mazingira ya kufanyia kazi na usimamizi wa maslahi ya watumishi, hali ya Ulinzi na Usalama, Utawala wa Sheria na Mapambano dhidi ya Rushwa, pamoja na changamoto na hatua zilizochukuliwa.

Taarifa ilipokelewa na Mwenyekiti alikaribisha majadiliano. Katika kujadili taarifa hiyo, wajumbe walishauri kuwa, Mkurugenzi Mtendaji Wilaya aandae mikakati itakayosaidia kuboresha Ofisi za kufanyia kazi hasa kwa ngazi za Vijiji, kwa mfano, kuna Vijiji vimeanzisha ujenzi wa Ofisi na zipo katika hatua nzuri, Vijiji kama hivyo Halmashauri isaidie angalau kupeleka vifaa vya ujenzi vilivyo nje ya uwezo wa wananchi wanaojitolea.

Aidha, wajumbe walipendelea Kamati ya Fedha, Utawala na Mipango wapewe taarifa sahihi ya kimaandishi kuhusu upanuzi wa chumba kimoja cha Ofisi na ujenzi unaoendelea kwa sasa Makao Makuu ya Halmashauri kama kuna wafadhili walíosaidia watajwe. Kaimu Mkurugenzi Mtendaji alitoa maelezo ya hoja za hapo juu.

Kuhusu Halmashauri kusaidia Vijiji vinavyojitolea ujenzi wa Ofisi alieleza kuwa suala hilo litaingizwa kwenye badjeti zijazo. Pia suala la upanuzi wa Ofisi alieleza kuwa, Mkurugenzi Mtendaji Wilaya alitoa maelekezo kwenye vikao vya awali. Baada ya majadiliano ya kutosha,

***ILIAZIMIWA*** kuwa,
(a) Mkurugenzi Mtendaji Wilaya kwenye bajeti ya mwaka 2022/2023 aweke kifungu kitakachosaidia fedha za ujenzi wa Ofisi za Vijiji (Vijiji vitakavyojitolea ujenzi vipelekewe vifaa vilivyo nje ya uwezo wao
(b) Mkurugenzi Mtendaji Wilaya aandae taarifa sahihi ya kimaandishi kuhusu upanuzi wa chumba kimoja cha Ofisi na ujenzi unaoendelea kwa sasa Makao Makuu ya Ofisi za Halmashauri

**KUMB. NA. 60/2021/2022 – MAOMBI YA KUBADILISHA MATUMIZI YA FEDHA TSHS 85,000,000/=**
Taarifa ya maombi ya kubadilisha matumizi ya fedha kiasi cha Tshs 85,000,000/= iliwasilishwa. Maombi hayo yaliwasilishwa kwa sababu Halmashauri ilitenga kiasi tajwa hapo juu kwa dhamira ya kulipa fidia kwa wananchi ambao wangeathirika eneo ambalo ingetengenezwa Barabara mpya kuendelea zinakojengwa Ofisi mpya za Makao Makuu ya Halmashauri.



Scanned with CamScanner

Barabara hiyo ingeanzia makutano ya Barabara kutoka Newala na Lindi kuelekea Masasi. Hata hivyo kwa vile zoezi la kulipa fidia linahitaji fedha zaidi ya Tshs 300,000,000/= (milioni mia tatu) kinaombwa kitumike kiasi cha Tshs 85,000,000/= (Milioni Themanini na Tano) kutekeleza mambo yafuatayo:-

1. Kulipa deni la mzabuni aliyesambaza bati kwenda katika Hospitali ya Wilaya Kiwalala Tshs 12,870,430/=
2. Gharama za kupima viwanja 500 eneo la Kituo cha Afya Mtama Tshs 17,840,000/=
3. Kurejesha fedha za SWASH Tshs 23,424,570/=
4. Gharama ya kuweka umeme katika Hospitali ya Wilaya Tshs 5,865,000/=
5. Gharama ya usimamizi wa miradi ya Halmashauri 25,000,000/=

Maombi yalipokelewa na Mwenyekiti alikaribisha majadiliano. Wajumbe walikubali kutoa idhini ya matumizi ya fedha maeneo mawili tu ambayo ni

1. Gharama za kupima viwanja 500 eneo la Kituo cha Afya Mtama Tshs 17,840,000/=
2. Gharama ya usimamizi wa miradi ya Halmashauri 25,000,000/=

Kwa hiyo jumla ya kiasi cha fedha kilichokubaliwa/idhinishwa ya matumizi ya fedha ni Tshs 42,840,000/=. Aidha, wajumbe hawakuwa tayari kutoa idhini ya matumizi kwa maeneo mengine kwa sababu hawakuridhika na maelezo yaliyotolewa ikizingatiwa kwamba Hospitali ya Wilaya huko nyuma kimepelekwa kiasi kikubwa cha fedha kwa mfano, walihoji kwa nini fedha za SWASH zilichukuliwa bila Kamati ya Fedha, Utawala na Mipango kupewa taarifa. Kwa hali hiyo,

***ILIAZIMIWA*** kuwa, Mkurugenzi Mtendaji Wilaya amepewa idhini ya matumizi ya fedha kwa ajili ya

(a) Gharama ya upimaji wa viwanja 500 eneo la ujenzi wa Kituo cha Afya Mtama Tshs 17,840,000/= (Milioni kumi na saba mia nane arobaini elfu tu)
(b) Gharama ya usimamizi wa miradi ya Halmashauri Tshs 25,000,000/= (milioni ishirini na tano)

**KUMB. NA. 61/2021/2022 – TAARIFA YA MAPOKEZI YA FEDHA TSHS 800,000,000/=**

Taarifa ya mapokezi ya fedha Tshs 800,000,000/= (Milioni mia nane) kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa Hospitali ya Wilaya iliwasilishwa.

Taarifa ilipokelewa na Mwenyekiti alikaribisha maoni ya wajumbe. Mjumbe Liveta alitoa maoni kwamba Mkurugenzi Mtendaji Wilaya akishirikiana na wataalam wakati wa kutekeleza mradi huo wawe wazalendo katika matumizi ya fedha za Serikali. Maoni hayo yaliungwa mkono na wajumbe wote.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji Wilaya alieleza kuwa, maoni ya wajumbe yatazingatiwa.

**KUMB. NA. 62/2021/2022 – TAARIFA YA MAPOKEZI YA FEDHA TSHS 1,250,000,000/=**

Taarifa ya mapokezi ya fedha **Tshs 1,250,000,000/= (Bilioni moja na milioni mia mbili hamsini)** ilipokelewa. Taarifa hiyo ilieleza kuwa, fedha hizi ni za mradi wa UVIKO – 19 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa madarasa Shule za Sekondari, vituo shikizi (kwa shule za msingi) pamoja na nyumba ya mtumimishi tatu kwa moja (three in one). Mchanganuo wa fedha hizi ni ufuatao:-

1. Ujenzi wa madarasa ya sekondari Tshs 760,000,000/=
2. Ujenzi wa vituo shiriki (shule za msingi) Tshs 400,000,000/=
3. Ujenzi wa nyumba ya mtumishi tatu kwa moja Tshs 90,000,000/=

Shule za sekondari ambazo zitatekeleza mradi wa UVIKO 19 ni zifuatazo:-

- Kiwalala Tshs 80,000,000/=



Scanned with CamScanner

- Mnolela Tshs 60,000,000/=
- Madangwa Tshs 80,000,000/=
- Mkopwe Tshs 60,000,000/=
- Mtua Tshs 60,000,000/=
- Nyengedi Tshs 60,000,000/=
- Mtama Tshs 80,000,000/=
- Mnara Tshs 60,000,000/=
- Nahukahuka Tshs 60,000,000/=
- Namupa Tshs 40,000,000/=
- Mahiwa Tshs 100,000,000/=
- Namangale Tshs 20,000,000/=

Aidha, fedha hizi zitatekeleza miradi ya ujenzi wa vituo shiriki kama ifuatavyo:-

- Mtemanje –Ujiranimwema Tshs 120,000,000/=
- Mawilo – Namangale Tshs 40,000,000/=
- Utimbula – Namangale Tshs 40,000,000/=
- Pangaboi – Nachunyu Tshs 40,000,000/=
- Mkung'uni – Navanga Tshs 40,000,000/=
- Namdeda – Mtua Tshs 40,000,000/=
- Kilidu – Nyangamara Tshs 40,000,000/=
- Mnazimmoja – Malungo Tshs 40,000,000/=

Taarifa ilipokelewa na Mwenyekiti alikaribisha majadiliano. Baada ya majadiliano ya kutosha wajumbe walipongeza Serikali ya awamu ya sita ya **Mhe. Samia Suluhu Hassani Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** kwa jitihada kubwa anazochukua kupambana na ugonjwa wa UVIKO – 19. Hivyo taarifa ilikubaliwa na kupitishwa.

**KUMB. NA. 63/2021/2022 – KUFUNGA KIKAO**

Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa majadiliano mazuri. Alisisitiza suala la ushirikiano kati ya waheshimiwa Madiwani, Mkurugenzi Mtendaji na wataalam katika kutekeleza shughuli mbalimbali za Halmashauri.

Aliwatakia wajumbe safari njema. Alifunga kikao saa 6.00 mchana.

PP ..............................
GEORGE E. MBILINYI
KATIBU

UMETHIBITISHWA

TAREHE 29/12/2021

..............................
YUSUFU ABDALLA TIPU
MWENYEKITI

MKURUGENZI MTENDAJI (W)
HALMASHAURI YA WILAYA
MTAMA



Scanned with CamScanner